# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuendelea kutukarimu neema ya uhai na afya njema sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa hali ya amani na utulivu. Aidha naendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa kujadili Bajeti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu mkubwa ili tuweze kuichangia kwa umakini na hatimae tuipitishe Bajeti iliyopo mbele yetu kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi

kwa kuiongoza vyema nchi yetu. Amani na utulivu wa hali ya juu ndani ya visiwa vya Zanzibar ambao unaendelea kudumishwa na uongozi wake ndio chachu ya maendeleo ya nchi yetu hususani katika ukuaji wa sekta ya utalii.

Aidha, pongezi pia ziwaendee Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah kwa namna wanavyoshirikiana vyema na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuhakikisha wanawaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa baraza, kwa jitihada zenu na namna mnavyoliongoza baraza hili tukufu kwa umakini na ufanisi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nitumiye nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi, kwa vile asilimia kubwa ya pato la nchi yetu linatokana na sekta hii ya utalii. Aidha, Kamati inatoa shukurani kwa Katibu mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili fungu la bajeti la Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kushiriki vyema katika kazi ya kupitia mapendekezo ya Bajeti hii kwa umakini na umahiri wa hali ya juu katika kutoa michango yao yenye lengo la kuhakikisha kuwa, sekta ya utalii inaimarika na kuleta maendeleo katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena niwatambue kwa majina wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii inafanya kazi zake kwa kuratibiwa na makatibu watatu na msaidizi mmojaa mbao ni:

1. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kasim - Katibu
3. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara katika jitihada zake za ukusanyaji wa mapato ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tsh, 775,068,586 sawa na asilimia 77.5 ya makadario ya Tsh. 1,000,000,000 ambayo yamekusanywa hadi kufikia machi 2024. Aidha Tsh. 224,931,414 sawa na asilimia 22.5 ni bakaa ya makusanyo ambapo kwa kipindi cha robo ya mwisho matarajio yetu makubwa ni kuwa kiwango hicho kitaweza kukusanywa na Wizara na kuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa asilimia mia au Zaidi ya hapo.

Hatua hii inadhihirisha wazi uwajibikaji na utendaji bora wa Wizara hii kwa watendaji wake, katika kufuata miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali hasa ile ya kuongeza wigo ukusanyaji wa mapato ndani ya taasisi zetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mbali na pongezi hizo Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuendelea kubunui vyanzo vipya vya mapato, kwa vile sekta ya utalii inazidi kuimarika kila uchao na idadi ya watalii kuongeza maradufu. Hivyo basi, ongezeko hilo la watalii halina budi kwenda sambamba na ongezeko la mapato katika sekta hii, kwa kuyadhbiti mapato hayo kwa kutumia njia mbalimbali za kielektroniki na kutumia mifumo ya Tehama kwa kuwatambua wageni wote wanaofika Zanzibar pamoja na hoteli wanazofikia. Hatua hii italeta ufanisi mkubwa katika kuongeza mapato katika nchi yetu kupitia sekta ya utalii.

**Programu kuu ya Kuratibu na kusimamia Maendeleo ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalenga kuleta mageuzi katika maendeleo ya sekta ya utalii ili kuweza kufikia lengo kuu la kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya Nchi na Wananchi. Nimelisema hili kwa vile Programu hii imeweza kutenga jumla ya Tsh. 1,152,962,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 75 ya makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika programu hii.

Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii na inataka kutekeleza ipasavyo shughuli zilizopangwa katika programu hii zikiwemo ushiriki wa jamii katika kuendeleza utalii, kutangaza vivutio vya utalii nchini na nje ya nchi na kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya kitalii kupitia kitengo cha polisi utalii na diplomasia.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa upekee naomba niipongeze Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa jitihada zake kubwa za kuutangaza utalii wetu wa Zanzibar katika masoko mbalimbali ya Nje ya Nchi. Idadi kubwa ya watalii inayomiminika Zanzibar kila uchao ni ishara kuwa kazi kubwa inafanyika kupitia Kamisheni na kuhakikisha kuwa utalii wa Zanzibar unakuwa kwa kasi na mapato yanayotokana na utalii yanazidi kuongezeka kupitia taasisi hii.

Kamati inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Kamisheni ya utalii na kuitaka kuongeza kasi ya utendaji wake ili azma ya Serikali ya kuongeza ajira na kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar kupitia sekta ya utalii iweze kutimia.

**Programu Kuu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe**

**Mheshimiwa Spika,**

Niendelee kuipongeza Wizara hii kwa kuona umuhimu wa kuyatunza na kuyaendeleza maeneo mbalimbali ya kihistoria visiwani Zanzibar ili kukuza utalii wetu na kuongeza pato la nchi.

Kwa mwaka wa fedha **2024/2025** programu hii imetengewa jumla ya **Tsh. 42,625,419,000** sawa na Ongezeko la asilimia **322.8** ya makadirio ya matumizi ya **Tsh. 10,080,499,000** kwa mwaka wa fedha **2023/2024.**

**Mheshimiwa Spika,**

Ongezeko hili la matumizi kwa program hii linaashiria kwenda kutekeleza kwa kasi miradi mbalimbali ya uimarishaji wa maeneo ya kihistoria ambayo

kwa mwaka wa fedha **2023/2024** miradi hiyo utekelezaji wake umeonekana kusuwa suwa kutokana na changamoto ya uhaba wa upatikanaji wa fedha Serikalini.

Kamati inaiomba Wizara kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo ili miradi iliyolengwa kuweza kukamilika ipasavyo na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana. Aidha, Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inawapa kazi za ujenzi wakandarasi ambao wana uwezo wa kifedha kwa lengo la kukamilisha miradi wanayopewa kwa wakati kwa kutumia fedha zao wenyewe pindi Serikali inapokabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha.

**Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji**

**Mheshimiwa Spika,**

Proramu hii inajukumu kubwa la kusimamia mipango, sera, na tafiti mbali mbalimbali za Wizara kwa lengo la kuhakikisha sekta ya utalii nchini inaimarika ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imetengewa jumla ya Tsh. 3,254,612,000.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vyema Programu hii, kwa vile hadi kufikia Machi 2024, Wizara imeweza kukamilisha rasimu ya awali ya Sera ya utalii ambayo kwa kiasi kikubwa itaweza kusaidia katika usimamizi wa utalii nchini pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko kasi ya teknolojia duniani. Aidha Wizara imeweza kufanya ziara mbalimbali za ukaguzi wa miradi ya kuimarisha maeneo ya kihistoria katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar inayotekelezwa kupitia Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Mbali na mafanikio hayo yaliyopatikana kupitia program hii, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watendaji wa Wizara hii kwa vile wao ndio watekelezaji wakuu wa shughuli za Wizara ambazo kwa kiasi kikubwa zinahitaji ufanisi na weledi katika utekelezaji wake, ikiwemo usimamizi wa miradi, ukusanyaji wa mapato na shughuli za uendeshaji wa Afisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuiarifu Wizara kuwa, shughuli ya kuendeleza sekta ya utalii ni kubwa na inahitaji watendaji wenye ujuzi, weledi na juhudi ili shughuli zilizopangwa ndani ya Progamu Kuu zote za Wizara ziweze kutekelezwa kwa kufikiwa malengo yake na hatimae tegemeo la mapato katika sekta ya utalii Zanzibar huenda likazorota.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watumie fursa hii kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale waliyojipangia kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati yangu naiunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

…………………….

Mhe. Said Saleh Salim,

Kny: Mwenyekiti,

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**